JEHOVAH JIREH LEARNING CENTER

SHULE YA AWALI NA MSINGI

Simu: +255 711 383 363 / 0757 509 993
Barua pepe: info@jehovajirehlc.co.tz | Tovuti: www.jehovajirehlc.co.tz
Vikonje A, Dodoma
Kauli mbiu: Elimika, Ukasaidie Jamii Yako

Hongera kwa Mzazi/Mlezi: _____

Tunawashukuru kwa kutuamini na kutukabidhi malezi na elimu ya mwanao. Tunathamini ushirikiano wenu. Mungu awabariki sana.

MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE

A. UTANGULIZI

Kwa kutambua uwezo na vipaji vilivyofichika ndani ya watoto yatima, watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi na watoto wengine, Jehovah Jireh Learning Center (JJLC) imejipanga kutoa fursa ya elimu kwa watoto wote kwa usawa. Tunawalenga kuwaandaa kielimu kuanzia elimu ya awali na msingi, ili waweze kuendelea na elimu ya sekondari na hatimaye elimu ya juu.

Tunaamini kuwa uwezo wa mtoto unapolelewa katika misingi ya maadili mema, elimu bora na mafundisho ya KiMungu, mtoto huyo anaweza kuwa baraka na mchango muhimu kwa jamii ndani na nje ya nchi.

Katika JJLC, tumejizatiti kutoa elimu bora na malezi yenye maadili mema ili kumwezesha kila mwanafunzi kukuza uwezo wake na kuwa mtu mwenye manufaa kwa jamii.

Kumbuka: Ni rahisi zaidi kuhamisha na kupanda mche mchanga kuliko mti uliokomaa. Vivyo hivyo, mtoto anapojengewa misingi imara ya elimu na maadili tangu akiwa mdogo, huwa rahisi kuyazingatia na kuyatumia katika mazingira mbalimbali atakayokutana nayo.

B. AINA YA SHULE

JJLC ni shule binafsi yenye dhamira ya kuchangia maendeleo ya jamii kwa kutoa huduma bora za elimu. Shule inatoa elimu ya awali (Nursery/Pre-Primary) na elimu ya msingi. Tunapokea watoto kuanzia umri wa miaka mitatu (3). Elimu na malezi yanayotolewa yanazingatia maadili mema na misingi ya Kikristo.

Shule inapokea wanafunzi wa kike na wa kiume bila ubaguzi.

JJLC ni shule inayotumia lugha ya Kiingereza (English Medium School). Lugha ya Kiingereza hutumika katika ufundishaji na mawasiliano ya shule. Aidha, somo la Kichina na Kifaransa hufundishwa kuanzia Darasa la Kwanza.

MAHALI SHULE ILIPO

Shule ipo Mkoa wa Dodoma, Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Kata ya Mtumba, Mtaa wa Vikonje ‘A’, jirani na Zahanati ya Vikonje. Ipo upande wa mashariki wa barabara inayoelekea Chuo cha Serikali za Mitaa, Hombolo.

C. ADA YA SHULE

Ada ya shule kwa kila ngazi ni kama ifuatavyo:

Ngazi ya Elimu	Ada kwa Mwezi	Ada kwa Mwaka
Elimu ya Awali	TSh 40,000	TSh 480,000
Kuanzia Darasa la Kwanza	TSh 60,000	TSh 720,000

D. MIHULA NA UTARATIBU WA MALIPO YA ADA KWA MWAKA

I. ELIMU YA AWALI (PRE-UNIT)

Muhula / Awamu	Kipindi	Kiasi
Muhula wa Kwanza – Awamu ya Kwanza	Januari hadi Machi	TSh 150,000
Muhula wa Kwanza – Awamu ya Pili	Aprili hadi Juni	TSh 150,000
JUMLA YA MUHULA WA KWANZA		**TSh 300,000**
Muhula wa Pili – Awamu ya Tatu	Julai hadi Septemba	TSh 90,000
Muhula wa Pili – Awamu ya Nne	Oktoba hadi Desemba	TSh 90,000
JUMLA YA MUHULA WA PILI		**TSh 180,000**

II. DARASA LA KWANZA NA LA PILI (CLASS I & II)

Muhula / Awamu	Kipindi	Kiasi
Muhula wa Kwanza – Awamu ya Kwanza	Januari hadi Machi	TSh 200,000
Muhula wa Kwanza – Awamu ya Pili	Aprili hadi Juni	TSh 200,000
JUMLA YA MUHULA WA KWANZA		**TSh 400,000**
Muhula wa Pili – Awamu ya Tatu	Julai hadi Septemba	TSh 160,000
Muhula wa Pili – Awamu ya Nne	Oktoba hadi Desemba	TSh 160,000
JUMLA YA MUHULA WA PILI		**TSh 320,000**

KUMBUKA: Ada za watoto yatima hulipwa na shule.

MALIPO YA ADA: Ada inalipwa kupitia Benki ya NMB kwa kutumia taarifa zifuatazo:

Namba ya Akaunti: **50210022596**
Jina la Akaunti: **DAVID STANLEY CHILEWA**

Taarifa muhimu: Mzazi/mlezi anatakiwa kuwasilisha stakabadhi ya malipo ya benki (Pay-in Slip) shuleni.

E. USAFIRI WA SHULE NA GHARAMA ZAKE

Huduma ya usafiri wa shule inapatikana. Gharama hulipwa kwa mwezi au kwa mwaka kulingana na eneo analotoka mwanafunzi, kama inavyooneshwa kwenye jedwali lifuatalo:

Eneo / Mtaa	Nauli kwa Mwezi	Nauli kwa Mwaka	Ada + Nauli kwa Mwaka (Awali)	Ada + Nauli kwa Mwaka (Darasa I)
Vikonje	TSh 67,500	TSh 810,000	TSh 1,290,000	TSh 1,530,000
Chahwa, Mtumba na Mahoma	TSh 75,000	TSh 900,000	TSh 1,380,000	TSh 1,620,000
Chamwino, Buigiri na Msanga	TSh 90,000	TSh 1,080,000	TSh 1,560,000	TSh 1,800,000
UDOM, Dodoma Mjini	TSh 150,000	TSh 1,800,000	TSh 2,280,000	TSh 2,520,000
Nzuguni, Veyula na Msalato	TSh 120,000	TSh 1,440,000	TSh 1,920,000	TSh 2,160,000

KUMBUKA: Mzazi/mlezi anatakiwa kuwasilisha stakabadhi ya malipo ya benki (Pay-in Slip) shuleni.

F. SARE ZA SHULE

Sare ya shule ni sketi au suruali ya kitambaa cha drafti ya Kimasai kilichochanganywa na rangi ya njano ya yai. Shati ni la rangi ya njano ya yai, lenye mapambo ya rangi inayolingana na sketi au suruali kwenye mikono na sehemu ya vifungo. Mwanafunzi anatakiwa pia kuvaa viatu vyepesi na soksi nyeupe.

Sare zinapatikana shuleni kwa gharama zifuatazo:

Aina ya Sare	Gharama
Shati na sketi/kaptula	TSh 30,000
Sweta la shule (rangi nyeusi)	TSh 15,000
T-shirt ya shule (rangi ya bluu bahari)	TSh 10,000
Tracksuit ya bluu	TSh 25,000
JUMLA	**TSh 80,000**

G. RATIBA YA UVALIAJI WA SARE

Siku	Aina ya Mavazi
Jumatatu, Jumanne na Alhamisi	Suruali/sketi na shati la shule
Jumatano	T-shirt ya shule na sketi/kaptula
Ijumaa	Tracksuit ya shule

H. TARATIBU NA SHERIA ZA SHULE

1. Watoto wanaotumia usafiri wa shule watachukuliwa na gari la shule kuanzia saa 1:00 asubuhi na kurudishwa saa 8:00 mchana. Wazazi/walezi wa watoto wasiotumia usafiri wa shule wanapaswa kuwafikisha na kuwachukua watoto kwa muda uliopangwa na shule.
2. Wazazi/walezi wanapaswa kuhakikisha kuwa watoto wanakuwa na viatu vyeusi na soksi nyeupe, pamoja na vifaa vya kujifunzia vilivyoainishwa hapa chini:
3. Kwa Darasa la Awali: Penseli za HB mbili (2); madaftari matano (5) ya kurasa 100 (daftari moja la kuchorea/ lisilo na mistari, madaftari matatu yenye mistari mikubwa na midogo, na daftari moja lisilo na mistari); kichongeo, rula na kifutio.
4. Kuanzia Darasa la Kwanza: Madaftari tisa (9), kichongeo, rula na kifutio.
5. Mzazi/mlezi anatakiwa kulipa ada ya shule kabla mwanafunzi hajaanza masomo.
6. Shule itafanya vikao vitatu (3) kwa mwaka. Wazazi/walezi wote wanatakiwa kuhudhuria vikao hivyo.
7. Kila mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria masomo siku zote zilizopangwa na shule.
8. Mzazi/mlezi anatakiwa kuomba ruhusa shuleni endapo mwanafunzi hatohudhuria masomo kwa sababu maalumu.
9. Mwanafunzi haruhusiwi kuja na chakula au fedha yoyote shuleni.

KARIBU SANA JEHOVAH JIREH LEARNING CENTER!

Elimika, Ukasaidie Jamii Yako